REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Tuesday, 23rd December, 2025

The House met at the Assembly Chamber at 10.12 a.m.

[The Speaker (Hon. Lantano Nabaala) in the Chair]

PRAYERS

QUORUM CALL

Speaker: Clerk, confirm if there is quorum.

(Lack of quorum confirmed)

Speaker: Without quorum, I direct that the bell rings for ten minutes.

(Quorum bell rang for five minutes)

Hon. Veronica Ikunyua: Thank you, Mr. Speaker. I can confirm there is quorum.

Speaker: Clerk, you can confirm if in deed we have quorum.

(Clerk confirmed achievement of Quorum)

Speaker: Thank you. Now that we have quorum, I direct that the bell stops ringing. Without much ado we proceed, to execute the orders of the day.

NOTICE OF MOTION

ESTABLISHMENT OF A COUNTY HUDUMA CENTRE

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you, Hon. Speaker. I beg to give notice of the following motion;

THAT, AWARE THAT Article 6(3) of the Constitution of Kenya guarantees access to public services in all parts of the country;

FURTHER AWARE THAT effective service delivery is a key pillar of devolution;

CONCERNED THAT many Laikipia residents face delays and high costs in accessing County services due to centralization;

APPRECIATING THAT timely provision of bursaries can enhance access to technical education, improve retention, and promote equitable participation in skills development across the County;

This House URGES the County Government to;

1. Establish a County Huduma Centre to serve as a one-stop point for County services in all the three Sub Counties.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

2. Decentralize key services to Sub-County levels to enhance accessibility and efficiency.
3. Allocate necessary funds and collaborate with relevant National Agencies to implement the initiative.

Thank you, Hon. Speaker.

MOTION

ESTABLISHMENT OF A COUNTY HUDUMA CENTRE

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you, Hon. Speaker. I beg to move the following motion;

THAT, AWARE THAT Article 6(3) of the Constitution of Kenya guarantees access to public services in all parts of the country;

FURTHER AWARE THAT effective service delivery is a key pillar of devolution;

CONCERNED THAT many Laikipia residents face delays and high costs in accessing County services due to centralization;

APPRECIATING THAT timely provision of bursaries can enhance access to technical education, improve retention, and promote equitable participation in skills development across the County;

This House URGES the County Government to;

1. Establish a County Huduma Centre to serve as a one-stop point for County services in all the three Sub Counties.
2. Decentralize key services to Sub-County levels to enhance accessibility and efficiency.
3. Allocate necessary funds and collaborate with relevant National Agencies to implement the initiative.

Bwana Spika, kama nilivyoeleza katika Bunge, kazi zetu katika Bunge hili wakati tulichaguliwa na wananchi ni tatu ambazo ni *representation*, *legislation* na *oversight*. Bwana Spika, kwa hii ninaongea mambo ya kuwakilisha kwa sababu sisi kama wajumbe wa Kaunti ni jukumu letu kuhakikisha ya kwamba tumewakilisha *Wanjiku* ipasavyo kwa sababu tulipewa na *Wanjiku* tuje hapa tumtetee, tumfanyie kazi na tuhakikishe ya kwamba mahali amekaa panastahili na anapewa huduma ambazo anastahili kupewa na serikali.

Bwana Spika, mambo ambayo ninaongea hapa ni kuhusu kituo cha huduma. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa, vituo vya huduma vilipoanzishwa na Rais mstaafu Mwai Kibaki ilikuwa ni maono mazuri. Aliweza kufikiria vile tutaweza kusaidia mwananchi katika Serikali Kuu. Bwana Spika, leo tunapoongea, ukitaka kitambulisho unaingia kituo cha huduma na kupata barua ya polisi (OB), hapo unapata *portal* na kitambulisho bila kutoka na kuelekea kwa polisi na ofisi tofauti.

Bwana Spika katika kituo kimoja, unasaidika. Bwana Spika, hata ukitaka kulipia KRA unalipia hapo. Ukitaka kuchukua cheti cha kuzaliwa unachukua hapo. Bwana Spika, wakati Rais Mwai Kibaki alikuwa Rais katika Jamhuri ya Kenya alikuwa na maono mazuri ambayo yaliweza kutimizwa katika Serikali Kuu. Tumekuwa na Serikali ya Ugatuzi wakati wa uongozi wake Bwana Spika wakiwa na marehemu Raila Amollo Odinga na Mungu amulaze mahali pema peponi walifikiria ugatuzi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Bwana Spika, madhumuni ya ugatuzi ni kuhakikisha ya kwamba huduma ambazo ziko katika Serikali Kuu zimeguza mwananchi wa kawaida. Bwana Spika, ndio maana tumeona katika Laikipia yetu, mwananchi ambaye anakaa Laikipia anateseka. Bwana Spika, Mtu akitaka kulipa leseni ama kupata huduma ya Kaunti akiwa Matanya ama Solio inambidi atoke huko na kuja hapa.

Bwana Spika, ili apate idhini ya kujenga nyumba ya mawe, siku hizi wanafanya kazi wakiwa wamejitolea. Sehemu nyingi wamepata maji ya kulima. Bwana Spika, huyo mtu akiuza kitunguu apate pesa, anaboresha nyumba yake kwa kujenga nyumba ya mawe. Bwana Spika, unaelewa sheria ambayo iko kwamba ukitaka kujenga nyumba ya mawe ni lazima upate idhini katika Idara ya Miundo Mbinu.

Hebu fikiria, mwananchi ambaye nimetaja kutoka huko akitumia pesa na muda wake kuja hapa ili kupata hiyo idhini. Bwana Spika, si huyo peke yake. Angalia mwananchi ambaye ametoka Chumvi karibu na Isiolo mahali ambapo Mheshimiwa Leshuel anawakilisha. Ili huyo mwananchi apate huduma inambidi kuja hapa. Mwananchi ambaye yuko Salama anatoka Kiamariga, Salama ili aende Nyahururu ama Rumuruti. Hata akienda huko anaweza kufika na kuambiwa aende Nanyuki. Tunatumia pesa na muda mwingi ili kupata hizo huduma.

Bwana Spika, ndio maana ninauliza serikali tuwe na *one-stop building*. Hata hivyo, huyo mwananchi akija hapa kupata idhini anasikia ni lazima alipie pesa katika Serikali ya Kaunti. Bwana Spika, ukitoka hapo unaingia ofisi ya kulipia kodi. Unatoka hapo na kuambiwa kuna pesa unafaa kulipia NEEMA. Inakubidi kutembea tena mpaka kwa ofisi ya DC. Unatoka hapo na kuambiwa kuna muhuri ambao unapigwa na mhandisi ya miundo mbinu.

Yeye yuko kona nyingine. Inakubidi uchukue bodaboda na kutumia pesa ingine. Bwana Spika, haya ni mambo ambayo yanasumbua mwananchi wa kawaida ambaye ametoka mbali. Mimi nimetoka Sweetwaters katika Wadi ya Thingithu. Mwananchi anafaa akifika hapa mambo yake yanyooshwe kwa muda mfupi na kurudi nyumbani kufanya kazi zingine. Utapata mtu ametoka baraka ambaye anataka idhini ya kujenga nyumba, anakuja hapa na kuambiwa aende katika ofisi ya miundo mbinu. Kisha anaambiwa alete barua ya NEMA.

Anatoka nje na kuja katika Ofisi ya DC na kupata barua. Bwana Spika, akitoka hapo anaambiwa bado hajakamilisha. Anatumwa kulipa katika ofisi ya kulipia kodi. Anatoka hapo na kwenda kutafuta Kamunya na kulipa. Bwana Spika, akitoka hapo anatumwa kwa mbunifu ili apate muhuri. Bwana Spika, hizo ni ofisi tofauti ambazo zimetawanyika kila mahali. Bwana Spika, ndio maana tunasema ni lazima tufanye kazi ya Representation.

Mwananchi akiingia ofisi moja, anafanyiwa kazi zote na kumaliza ili akafanye biashara nyingine. Bwana Spika, wakati mwananchi anazunguka hapa, hakuna kitu serikali inamlipa. Yeye ndiye anagharamia serikali. Bwana Spika, mwananchi alinipigia kura ili nimwakilishe. Matatizo kama haya anapata, nihakikishe yameisha. Ndio maana leo nimesema ni lazima tuwe na kituo cha huduma ambapo mwananchi atalipia huduma zote hapo. Bwana Spika, tunafaa kuwa na vituo za huduma katika kata ndogo. Kama tuko nayo katika Mashariki mwa Laikipia iwekwe katikati kama Matanya.

Hii ni kwa sababu ukisema ya kwamba yule mwananchi atatoka Ngobit aje hapa Nanyuki, bado hatujampatia nafasi nzuri ama hatujaangalia maslahi ya pesa zake ambazo atatumia. Tunataka iwekwe katikati. Vile vile, katika upande wa Laikipia Kaskazini, tunataka wawe na mahali maalum ambapo mwananchi akifika pale anaweza kupata hizo huduma.

Bwana Spika, katika upande wa Laikipia Magharibi, tunataka tuwe na mahali *central point* ambapo mwananchi atakuwa anapata hizo huduma. Jambo la tatu, ni lazima tuungane na

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

National Governmnet Agencies kwa sababu huduma zingine zinahitaji Serikali Kuu kama NEMA. Kwa hivyo, ni lazima tuwe na hizo ofisi katika *sub counties* zote. Kwa sababu iko hapa ni kuagiza tu kutoka kwa wizara ili kuteua watu watatu ambao watasimamia na wananchi wataweza kupata huduma za serikali wa haraka.

Bwana Spika, hayo ndiyo maoni yangu na ndio nimetumwa na wanjiku na kuniambia ya kwamba anateseka. Anafaa akifika mahali anafanya kazi yake na kuimaliza. Ili nilete huu mjadala, nimekuwa nyumbani kwa likizo ya wiki mbili ambapo nilipata mazungumzo na wananchi kila siku. Wakati mwingine niliongea na wananchi hadi saa tisa ya usiku tukijaribu kupanga vile Thinghithu itakuwa sawa sawa. Hapo ndipo waliniambia ya kwamba wanateseka sana. Kwa hivyo, ni jukumu langu kuleta huu mjadala hapa ili kutetea na kuomba hawa Wajumbe tuungane ili tuweze kusaidia wananchi wa Laikipia nzima.

Bwana Spika, mimi nafurahishwa na haya mambo ya *huduma centre.* Saa hivi, tuko na *huduma centre* katika Ngobit ambayo inasaidia watu kwa njia kubwa sana. Hebu tafakari vile mwananchi wa Ngobit alikuwa anakuja hapa Nanyuki ili aweze kupata cheti cha kuzaliwa? Hiyo ilikuwa ni dhuluma ya hali ya juu kwa mwananchi. Vile vile, ili tuweze kuwa na huduma za serikali ya Kaunti ili vitu kama leseni unalipia mahali ambapo uko. Ikiwezekana, kila kitu iwe digitali ili ukiwa nyumbani unafinya tu simu yako au kompyuta ili mambo yote iwe sawa sawa.

Mimi najivunia Rais wa Kenya kwa sababu sasa nimeona amechukua mkondo mwingine wa kututoa *bottom up.* Amekuja kwa njia nyingine kwa sababu sasa anataka kutubadilisha tuwe kama Singapore ambapo hayo ni maono ya juu. Hata hapa tunataka tuwe kama Singapore ambapo tuna maendeleo na huduma katika kila kona. Ninaomba wakati ambapo tutaenda kupiga kura, pia tuwe waangalifu sana tusije tukapita kwa mambo ya *wheelbarrow* na *bottom up* halafu tunajipata kwa shida.

Sasa hii Singapore sijui kama itakuwa kama ni ile Singapore ya ukweli ama ni Singapore ya kutafuta kura. Kura zitafutwe lakini zitafutwe kwa njia ya ukweli. Hapo mimi nasema, naangalia, nitapima na kuchungulia kabisa ili niweze kujua kwamba mwananchi wetu anachezwa ama ni ukweli. Kama ni ukweli, namuunga mia kwa mia ili tuweze kubadilisha nchi yetu iwe kama Singapore ndogo. Kwa hayo machache, nataka kuuliza Mheshimiwa Mugambi Gatati kutoka Salama ambaye anaelewa maana ya kuwa na *central point* katika kila *sub-county*, maanake wadi yake iko na sehemu nyingi ambapo wananchi huishi mbali na kupata nauli tu inabidi mtu atumie zaidi ya elfu tatu.

Nilikuwa katika sehemu ya Mutara na nikaingia katika hoteli moja pale kando na nikapatana na mwananchi ambaye alikuwa anasema ya kwamba anataka kuendea kitambulisho Rumuruti. Mtu ako Mutara na anaendea Rumuruti na ni mtoto ambaye amemaliza shule. Kwa nini tusiwe na sehemu kama Pesi ambapo ni *central point* na mwanchi yeyote wa ile sehemu atapata huduma pale. Kwa hivyo ndio maana namuita kijana mkakamavu Samuel Mugambi Gatati. Naomba watu wa Salama, kama tutakosa huyu Mbunge katika Bunge ijayo, sijui itakuwa namna gani. Tunahitaji watu wa Salama wampigie kura kwa kishindo ndio tuwe na viongozi ambao wanaelewa mambo ya kuunga mkono na kuhakikisha ya kwamba wananchi wake wanasaidika. Asante, sana, ninamkaribisha Mheshimiwa Gatati.

Hon. Samuel Mugambi: Thank you, Hon. Speaker. I stand to second the motion on establishment of County Huduma Centre for decentralization of county services. I also want to echo the same words which our able chairman and the mover of the motion, Hon. Ndiritu echoed. That we need to establish a County Huduma Centre to serve us at one point for county services in all the three sub counties. We also decentralize key services to sub county levels to

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

enhance accessibility and efficiency. Also to allocate sufficient funds and collaborate with relevant national agencies to implement the initiative.

Hon. Members, this is a very important motion and if it can be implemented, we can solve a lot of problems that our people face. Very good examples that the mover has mentioned is the revenue services like licensing, the agriculture extension services, land search issues, transfer of plots, land rates, etc.

Mr. Speaker, Hon. Ndiritu has given an example that someone in Mutara to move from Mutara to Rumuruti is approximately 25 kilometers and the only offices he/she can access is Rumuruti or Nanyuki or Nyahururu. From Mutara to Rumuruti is 25 kilometers. From Mutara to Nanyuki is 75 kilometers and from Mutara to Nyahururu is also approximately 20 kilometers. Wards like Tigithi, Mukogodo and Ngobit, for them to access county services they need to travel either to Nanyuki or Nyahururu. You will even find so many people from Ngobit Ward travelling towards Nyahururu in Laikipia West and Ngobit is in Laikipia East.

This is a very timely motion and also the committees especially the Committee on Implementation also to follow up when it comes to budgeting so that we can start it from the stage of budgeting to implementation. There is also something which is very important that the mover has mentioned that after decentralizing the services to sub counties, we also need to digitize them so that our communities can be using the services from home. He has used a very good example of the way our President is saying that he wants to transform Kenya to Singapore.

I was a good student of history. The one thing that changed Singapore is technology and you cannot talk about development nowadays without talking about technology. As I am speaking here, all of you are using your phones and nobody is looking at me. That means that technology is strong because it affects our lives 24 hrs. You will find that for you to get all services like banking services, Mpesa services, and school fees. Some of the Members here are parents and therefore they receive some information about students through their phones.

Hon. Speaker, as we are talking about decentralization of county services, we also need to emphasize more on digitizing the services. For you to pay a license permit, if you are in Tigithi, you don't need to travel to Nanyuki but to access a sub county office on Tigithi or in Laikipia West Sub County and access using your phone. Recent introduction of AI because Hon. Ndiritu usually emphasizes more on AI. One time he was calling a Hon. Member here and nicknamed him AI.

Hon. Speaker, I think that we need to use a lot of technology even in delivering the services that we carry out in the Assembly. When Hon. Wachuka is seated here in Nanyuki, the people of Igwamiti Ward should know that Hon. Wachuka is here present and representing the people of Igwamiti. But you find that so many things we usually do here are not even broadcasted because of failure of technology and also the human error. So, as long as we are talking about the county services being decentralized, we also need to decentralize our services here in the County Assembly.

Even in our website because one way of accessing information is using website. I want to congratulate Hon. Ndiritu for this timely motion on establishment of County Huduma Centre. We purpose to follow up with the next budget and at least start with two sub counties that will have all the services that the county offers together.

(Question proposed)

Hon. Irene Wachuka: Asante sana, Bwana Spika. Nataka kushukuru Mheshimiwa Ndiritu ambaye ameleta huu mjadala. Umeniguza sana kwa sababu wakati alikuwa anaongea

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

nilikuwa nafikiria ya kwamba ni mimi ameona. Ningetaka kueleza Mheshimiwa Gatati kutoka Salama ya kwamba Nyahururu hatuna huduma. Sisi huja Makutano au Nyandarua. Juzi wakati nilikuwa nimepoteza bwanangu, katika shughuli za kutafuta huduma, hata niliongeleshwa vibaya na watu wa Nyandarua huko Ol Kalau. Walinikejeli na kusema ya kwamba tunafaa kuwa na huduma yetu na ya kwamba nilikuwa mtu wa kwanza kuwafukuza Nyahururu.

Kwa hivyo, naamini ya kwamba kuna wakati ambapo Mheshimiwa Ndiritu anaongeleshwa na Mungu kwa kufikiria ile shida ambayo iko katika Kaunti nzima. Laikipia Mashariki wamebahatika kupata huduma hapa Nanyuki na ingine huko Ngobit. Laikipia Kaskazini hawana na sijui ni kwa nini kila mtu akichaguliwa huwa anasahau Laikipia Kaskazini na hao huwa na kura kama zile zingine katika *sub-counties.* Mimi naomba tuunge huu mjadala na pia tuweze kuongea na Gavana ana kwa ana ili aweze kutuelezea ni nini ambacho kinaendelea. Wakati alikuwa kwa kiti mara ya kwanza, hatukupata na sasa ameingia mara ya pili na bado hatujapata huduma katika Laikipia Magharibi na Laikipia Kaskazini.

Laikipia Magharibi ujue ya kwamba ndio kama *head quarter* ya Laikipia na Nyandarua. Tayari, Nyandarua wameanza kuhama na tunangojea tu tupewe *charter* ya manispaa kwa sababu kila kitu ambacho walikuwa nacho wameanza kutoa.

Nataka kusema asante sana kwa Mheshimiwa Ndiritu kwa sababu wakati mimi nitapata *charter,* kuna shule mbili ambazo nitachukua Nyahururu ambazo zimeenda Nyandarua kama *Nyandarua boarding* na *Nyahururu high school* huko hostel. Hapo hata ndipo ningeuliza Gavana na Waheshimiwa wetu wapate kuona. Kama tutapewa *charter*, hakuna kujenga maanake kila kitu kiko kwa sababu wameanza kutoa kila kitu chao wakirudisha Nyandarua. Kwa hivyo, huu ni mjadala muhimu sana.

Napongeza pia Waheshimiwa ambo wamefika hapa na ni lazima tutafanya kazi na hatuondoki mpaka tuhakikishe ya kwamba tumetimiza ndoto ambayo tuliahidi wananchi. Tunashukuru pia Bwana Spika na wafanyikazi wote ambao wamefika. Ni watu wetu na wakati ambapo tunapongeza wengine, hatuwezi kufanya kazi bila hao. Kwa hivyo, asanteni sana na Mungu awabariki.

Hon. Paul Leshuel: Thank you, Mr. Speaker. I also stand to support the motion. I want to appreciate the mover of the motion; Hon. Stephen because it is very important to the entire population of Laikipia. As the mover mentioned, when we got the *huduma* center, in fact those who are near Nanyuki, the *huduma* center has really served us well.

Mr. Speaker, the reason as to why we came up with devolution, it is to devolve functions to people and therefore, it is important that we continue to devolve all services to the people. Services nearer to the people also benefits the economy. When Hon. Ndiritu mentioned the kilometers, some people travel to reach the services, what about people from Laikipia North who travel 60 to 70 kilometers in a day to get services? How much do they incur per day to get ID services and other services?

So, it is very important if the County Government can think critically and identify some of the services that can be decentralized to the sub counties. Before they talk with the National Government, we have got many staff in the County Government whom we can devolve to the sub-counties who will be serving g the people in sub county levels thus reducing the expenditures of our people in Nyahururu, Rumuruti and Nyahururu.

I agree with the Member that we need all these services closer to the people so that we can be able to serve our people in a better way. The reason as to why we have got leaders is not to go and give people income or create businesses for the people but to give them a

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

conducive environment to enable them to do things in the most achievable way. I agree that we need to talk with the national agencies and the County Government so that we can be able to decentralize services to the sub counties.

Services like AI services in agriculture, those services should be on the ground everyday so that we don't again travel here in Nanyuki. Today if you want to move your cattle from one place to another, you have to travel to Nanyuki to get a permit. Those are things we need to be having staff on the ground who can be giving those documents. Why do you have to travel to Nanyuki to come and get a receipt of Kshs.500 shillings when you have spent more than 3,000?

So, we need to properly analyze and get the right services that we need to decentralize and liaise with the National Government. I totally agree and we are going to follow this motion to the delivery point so that even if we will not be able to decentralize to 100%, we can deliver almost 50% in a very simple way without incurring a lot of cost. I want to appreciate the Member for coming up with this important motion which touches all people and also will reduce a lot of cost to Laikipians. That is why we are leaders in this House representing them. That is why we need to know their needs and address them in a way that is supposed to be. Thank you.

Hon. Salim Edung: Asante sana, Bwana Spika kwa kunipatia hii nafasi. Kwanza ni kupongeza aliyeleta mjadala huu ambaye ni Mheshimiwa Ndiritu. Vile Mheshimiwa Wachuka amesema ya kwamba Mungu hutumia watu, ametumia Mheshimiwa Ndiritu kwa kuangalia kwa ufasaha sana ya kwamba kuna jambo ambalo linahitajika katika Kaunti yetu.

Tukijadili mambo ya huduma mashinani, watu wanafaa kuangaliwa kwa makini sana. Katika huu mjadala wa leo, bila kuungwa mkono na Mheshimiwa Gatati, pia halingekuwa mjadala. Kwa hivyo, nashukuru pia Mheshimiwa Gatati kwa kuafiki na pia Wabunge wote ambao wako hapa kwa sababu tumeletwa hapa ili tuwakilishe wananchi katika mashinani.

Vilevile, naipongeza serikali kuu kwa sababu iwapo wataendelea na mtindo ambao waliuanza hivi majuzi, hususan walipoleta ICT hub kwenye wadi zote; kama kituo cha Huduma Centre kitaletwa mashinani, hilo litakuwa jambo nzuri sana. Vilevile, itatoa nafasi za ajira kwenye eneo hilo. Huduma Centre ikiwekwa kwenye sehemu ya Doldol, vijana wanaotafuta kazi watapata kwenye hilo eneo. Vilevile, safari kutoka mbali itapungua.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa makini sehemu kama ya Nyahururu; na watu ni wengi kwenye hio sehemu; hakuna Huduma Centre. Hii inamanisha kuwa bado kazi nyingi imebaki kwenye ugatuzi, na kituo cha Huduma Centre kinahitajika kwenye hiyo sehemu ili kuwahudumia watu wa eneo hilo.

Jambo lingine ni kwamba fedha inahitajika. Ushirikiano kati ya Serikali ya Kaunti na Serikali ya Kitaifa unahitajika. Tunasema kuwa ugatuzi ni kuleta huduma mashinani. Hata hivyo, ni kama asilimia ishirini tu ya ugatuzi ndio imetekelezwa mashinani ilhali serikali kuu imebaki na asilimia themanini.

Serikali kuu na serikali za Kaunti zikishikana kuweka mikakati na kutenga pesa, huduma itakuwa rahisi kwa wananchi. Nilikutana na mzungu mmoja mwezi uliopita. Aliniuliza ni wapi ataenda kuchukua barua ya kulipa *land rates.* Nilimweleza kwamba lazima aje hadi Nanyuki kulipa. Alisema kuwa amesoma kwenye katiba ya Kenya kwamba kuna ugatuzi, ambayo inamaanisha kuwa kuna huduma hata mashinani. Huyo mzungu alisafiri kilometa takriban 68 kuja Nanyuki kulipa *land rates.* Hili linaonyesha kuwa bado tuna kazi na tunahitaji kuifanya ili kuwasaidia wananchi, maanake hao wananchi ndio walituleta hapa.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Bwana Spika, umetupa nguvu, nasi kama wawakilishi wa wadi tutafanya kazi jinsi ambavyo wananchi walituambia. Ndio maana siku ya leo, tarehe 23, tuko Bungeni. Sisi hatuna shughuli na Krisimasi, tunatekeleza tu kazi ambayo mwananchi alitupa. Natoa pongezi kwa sababu huu mswada umekuja wakati ambao unastahili. Tutakapofungua Februari mwakani, tunajua kwamba huu mswada uliopitishwa kwenye Bunge hili utafuatwa kwa makini ndiposa watu wetu wapate huduma kama wengine. Asante.

Speaker: Thank you, Hon. Salim. I now give the chance to the mover of the motion to reply.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante Bwana Spika, kwa kunipa hii nafasi ya kutoa jibu kwa huu mswada ulioletwa hapa siku ya leo ambao madhumuni yake, ni kuhakikisha kuwa mwananchi anapata huduma kwa karibu na kukingwa dhidi ya hasara anapoenda kutafuta huduma. Mwananchi anastahili kupata huduma za serikali bure bila gharama yoyote. Hio ndio maana tuko na zaidi ya idara nane kwenye kila pembe ya Kaunti yetu, ambazo zinafaa kutoa huduma kwa mwananchi. Tunao wafanyikazi wa kutosha ambao tunastahili kuwatuma hadi kwenye mlango wa mwananchi.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri uelewe kuwa tunayezungumza kumhusu hapa, apokee huduma, ndiye mkubwa wetu. Uongeapo na mkubwa, unafaa kuongea kwa heshima. Huyo ndiye mkubwa wetu. Kwa hivyo, tunapoleta mswada kama huu, tunajua kwamba tunaleta mswada unaomhusu mkubwa wetu. Kwa hivyo, tutaufuatilia huu mswada. Kama alivyosema Mheshimiwa Gatati, ambaye ndiye ameuafiki huu mswada, tutahakikisha kuwa Kamati ya Utekelezaji ikiongozwa na Mheshimiwa Shuel inahakikisha kuwa huu mswada unafanyiwa kazi.

Hatuleti mswada hapa ili kupaka tu rangi. Tunahitaji mwananchi aweze kupata huduma. Hatumfanyii hisani; ni haki yake. Wazia tu, Mheshimiwa Spika, mtu kusafiri kutoka kule mbali Mutara hadi Nanyuki kulipia leseni ya biashara. Hio ni madharau. Hatumpi huyu mkubwa wetu heshima anayostahili. Yeye anahakikisha tunalipwa tarehe moja ya kila mwezi, ila shida ni kuwa anayestahili kutulipa hatulipi, ilhali huyu mkubwa wetu amewachilia pesa mapema.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba hili Bunge letu, najua *Wanjiku* anatazama, linafanya kazi katika wakati wa ziada. Tunafanya kazi kupita kiasi. Hebu wazia, katika Kenya nzima hakuna Bunge lingine lililo kazini isipokuwa hili la Laikipia. Natoa pongezi, na mwananchi anajua ni yeye tunamfanyia kazi. Nastahili kuenda sherehe bali sijaenda ili nihakikishe kuwa namfanyia mwananchi kazi.

Mheshimiwa Spika, ili ujue hili Bunge linafanya kazi, hebu tazama hivi viti. Vimeisha. Vimeketiwa hadi vikararuka. Hili ni changamoto kwa wanaostahili kuvifanyia ukarabati. Tunavikalia tunapofanya kazi, na vikiraruka ni haki yetu vifanyiwe ukarabati. Mimi nimekuja na suti ambayo nimenunuliwa na mke wangu. Nilipokosa kulipwa, mke wangu aliuza kuku na kuninunulia suti. Hata ukiiangalia nyuma utaona imechakaa, hata sijui nitamwambia nini. Hayo ni mambo yanayostahili kushughulikiwa kwa wepesi.

Kwa hayo machache, nawapongeza Wabunge kwa kuunga mkono huu mswada, ili upitishwe na kufanyiwa kazi. Kesho tarehe 24 tutakuwa hapa. Mwokozi anazaliwa kesho jioni, kwa hivyo mimi nitatoka hapa kuenda kushuhudia Yesu akizaliwa. Yeye ni Mwokozi wa kuleta amani na kujali mambo ambayo sisi hatuyawezi. Anatulinda, na hata sasa hivi tunamwomba Mungu atufiche kwenye manyoya yake kama kuku ili tusipate shida yoyote. Nawatakia Wabunge wote Krisimasi njema na mwaka mpya wenye mafanikio. Mungu akitujalia wakati mwingine, tuje hapa tukijua kwamba sisi wote tumezaliwa ndani ya Kristo na sote tunampenda Kristo. Asanteni na Mungu awabariki.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Speaker: The sittings of this House now stand adjourned until later today, Tuesday, 23rd December 2025 at 2.30 p.m.

The House rose at 11.04 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*